*Kioo cha Lugha, Juz. 19(2), 2021, 39-50*
*Jarida la Taasisi ya Taaluma za Kiswahili*
*Chuo Kikuu cha Dar es Salaam*.

# Uhakiki wa Nadharia ya Fomula ya Kisimulizi katika Tamthilia ya *Jogoo Kijijini*

*Sophie Okwena*[1]

## Ikisiri

Makala hii imehakiki Nadharia ya Fomula ya Kisimulizi katika tamthilia ya *Jogoo Kijijini* (1976). Tamthilia ya *Jogoo Kijijini* imewasilishwa katika muundo wa fasihi simulizi. Waaidha, tamthilia hii imechota malighafi yake kutoka Afrika. Katika tamthilia hii ya kidrama, Ebrahim Hussein ametumia muundo wa kitendawili, ngano na shairi huru, ambavyo ni baadhi ya vipengele vya fasihi simulizi ya Kiafrika katika utunzi wake. Licha ya kwamba watafiti waliotangulia walihakiki tamthilia hii kwa kuegemea katika wahusika, maudhui na mtindo; suala la nadharia iliyotumika katika utunzi wa tamthilia hii halijashughulikiwa kwa kina. Hivyo basi, kulikuwa na haja ya kuchunguza matumizi ya Nadharia ya Fomula ya Kisimulizi katika tamthilia teule. Uchunguzi huu umeongozwa na Nadharia ya Fomula ya Kisimulizi. Azma ya kutaka kubainisha fomula za uwasilishaji ndiyo imechochea matumizi ya Nadharia ya Fomula ya Kisimulizi kwa lengo la kuziba pengo lililopo. Uhakiki huu umefanywa kwa lengo la kuchanganua Nadharia ya Fomula ya Kisimulizi katika tamthilia ya *Jogoo Kijiini*. Kimsingi, uhakiki huu umedhamiria kuthibitisha kuwa Nadharia ya Fomula ya Kisimulizi imetumika katika utunzi wa tamthilia ya *Jogoo Kijijini*.

## 1.0 Utangulizi

*Jogoo Kijijini* (1976) ni tamthilia ambayo imeandikwa kwa kutumia kunga za fasihi simulizi. Ebrahim Hussein aliandika tamthilia hii ambayo imejikita katika desturi ya utambaji hadithi na matumizi ya vitendawili. Aidha, ametumia ngano katika tamthilia yake ya *Jogoo Kijijini*. Mtunzi huyu hajatumia kunga hizi tu bali amezitumia kwa ubunifu wa hali ya juu na jinsi inavyostahiki (Njogu na Chimerah, 2011). Tamthilia hii inaweza kuchukuliwa kama utunzi ambao umetumia fomula ya kisimulizi katika uwasilishaji wake. Fomula ya kisimulizi hupatikana katika sanaa za jadi za Kiafrika. Pia, Ebrahim Hussein ametoa tamthilia yake kwenye muundo uliobadilika, changamani zaidi na usioeleweka kwa urahisi (Bertoncini, 1989).

[1] Mhadhiri wa muda, Idara ya Kiswahili, Kitivo cha Kiswahili na Lugha nyingine za Kiafrika, Chuo Kikuu cha Kenyatta, Nairobi, Kenya. Baruapepe: sophiejoyedwin@gmail.com

Tamthilia ya *Jogoo Kijijini* ni mfano wa tamthilia ambayo imeathiriwa sana na kunga za fasihi simulizi. Ebrahim Hussein ni mwandishi ambaye amerudisha mizizi yake Afrika kwa lengo la kutambulisha asili yake. Katika utamaduni wa Kiafrika, hadithi hutambwa na bibi aghalabu wakati wa magharibi au usiku baada ya chajio na baada ya shughuli za siku. Hadithi hizi hutoa maelezo, maonyo na maoni kuhusu matukio mbalimbali. Watoto na watu wazima humzunguka mtambaji kusikiliza hadithi inavyowasilishwa. Mara bibi huyu anaweza kubadilika na kuwa mhusika kwenye hadithi. Masimulizi haya ya kimapokezi yana fomula ya kuyawasilisha. Hii ni fomula ya kufungua na kufunga. Kuna dhima mbili kuu za fomula ya kufungua na kufunga katika hadithi. Kwanza, muundo huu wa uanzishaji na umaliziaji wa hadithi humtayarisha msikilizaji kuukubali mwanzo na mwisho bila taharuki. Pili, muundo huu unawafanya wasikilizaji wapae na kutua taratibu, na kwa jinsi hiyo, wanapofikia mwisho wa masimulizi hamu yao yote inakuwa imetimizwa na kuridhishwa wala hakuna taharuki inayobakia (Njogu na Chimerah, 2011).

## 2.1 Nadharia ya Fomula ya Kisimulizi

Kulingana na Dundes (1999), Nadharia ya Fomula ya Kisimulizi ilipendekezwa na Milman Parry mwaka 1939 na mwanafunzi wake, Albert Lord. Nadharia ya Fomula ya Kisimulizi ni tawi la naratolojia. Naratolojia ni istilahi ya kijumla ambayo ina matawi mengi. Kuna tawi la fomula ya kisimulizi ya Parry *(khj)* na Lord (1960) ambayo imejikita katika mashairi na nyimbo na pia kuna masimulizi sahili ya Propp (1968) na Olrik (1992) ambayo yamejikita katika hadithi. Katika makala hii, mwandishi ametumia tawi la masimulizi sahili ya Propp (1968) na Olrik (1992). Mtazamo wa Propp (1968) na Olrik (1992) umeteuliwa kwa sababu wataalamu hawa wameutumia katika misingi ya hadithi kwa kuwa tamthilia ya *Jogoo Kijijini* imeandikwa kihadithi.

Nadharia hii ilipambanuliwa kwa undani na Propp (1984), Olrik (1992) na Dundes (1999). Propp (1968) alitafiti kuhusu simulizi za jadi akilenga fomula na taratibu za masimulizi ya Urusi. Propp (1968) anasema kwamba kuna upekee wa fomula katika masimulizi ambao unapatikana katika kila aina ya simulizi. Naye Olrik (1992) anaongeza kwamba kuna maumbo yanayopatikana katika simulizi zote na kuna sifa bainifu za masimulizi ambazo zimetamalaki katika visakale, visasili, mighani na nyimbo. Sifa hizo ni: fomula ya kuanzisha na kumalizisha masimulizi, sifa ya urudiaji wa matukio, sifa ya dhima ya wahusika, na sifa ya ukinzano. Hii ina maana kwamba kuna kanuni ambazo zinatawala simulizi zote na kanuni hizi hazijadhibitiwa katika utanzu mmoja bali zinaweza kutumika katika tanzu nyingi.

Olrik (1992) alichunguza masimulizi ya kale hasa alipoangazia arudhi za utendi. Baadaye alitambua kuwa kuna fomula zinazopatikana katika simulizi zote. Kadhalika, Olrik alitaka kubaini iwapo kulikuwapo na miundo ya sifa bainifu za masimulizi zinazotofautisha fasihi andishi. Naye Dundes (1999) anasema kuwa Olrik aliona kwamba masimulizi fulani yalipoingia katika fasihi andishi yalielekea

kupoteza baadhi ya sifa bainifu za masimulizi. Dundes anaonesha kuwa mojawapo ya malengo muhimu ya Olrik na Propp yalikuwa kuthibitisha iwapo kulikuwapo na vigezo au sifa za masimulizi. Baadhi ya kanuni hizi walizobaini ni pamoja na: muundo wa kifomula wa kuanzisha au kufungua masimulizi na kumaliza au kufunga masimulizi, kanuni ya urudiaji wa matukio, dhima ya wahusika, kanuni ya ukinzano,mhusika nguli, matumizi ya nyimbo, na motifu ya safari. Kanuni hizi ndizo hatimaye ziliweka msingi wa mihimili yake. Kutokana na maelezo ya wataalamu hao, uchanganuzi huu umeongozwa na mihimili ya Fomula ya Kisimulizi ambayo ni: Fomula ya kufungua utambaji hadithi na fomula ya kuhitimisha utambaji hadithi. Fomula ya kufungua utambaji hadithi ni muundo maalumu wa kuanzisha hadithi. Fomula hii hutumika kuvuta umakini wa wasikilizaji kwa lengo la kuwaweka tayari kumsikiliza mtambaji. Fomula ya kuhitimisha utambaji hadithi ni muundo wa kumalizia hadithi. Fomula hii huonesha kuwa hadithi imefika kikomo hivyo kumpisha fanani na shughuli inayofuata.

### 3.1 Muhtasari wa Tamthilia ya *Jogoo Kijijini*

*Jogoo Kijijini* (1976) ni tamthilia inayoonesha mgogoro kati ya wenyeji na wakoloni ambao walipowasili Afrika wenyeji waliwapokea vyema. Baada ya wageni hawa kupokelewa, waligeuka na kuanza kuwakandamiza wenyeji wao. Kutokana na dhuluma hizi, kulizuka mgogoro mkubwa. Mwafrika alipoona haya, alianza kutafuta mbinu ya kujikomboa kutoka katika minyororo ya mkoloni. Hadithi inaangazia historia ya Afrika na jinsi bara hili lilivyopokea wageni, yaani wakoloni kwa moyo mkunjufu bila wao kufahamu hila zao (Njogu na Chimerah, 2011).

Ebrahim Hussein ameandika tamthilia yake ya *Jogoo Kijijini* akitumia muundo wa utambaji hadithi. Msanii huyu amesimulia hadithi hizi akianza na muundo wa '*paukwa pakawa*' na kumalizia katika mtindo wa kitendawili akiomba apewe mji ili afumbue fumbo.

### 3.2 Fomula za Ufunguzi na Uhitimishi

Fomula katika ngano ni mtindo maalumu wa kuanzisha na kumalizia hadithi. Kuna kanuni maalumu za kuanzisha na kumaliza masimulizi zinazofahamika kifomula (Olrik, 1992; Matei, 2011). Kanuni hizi ni muhimu sana katika simulizi zote kwa sababu huandaa hadhira kila mara hadithi inapoanza na inapohitimishwa.

Kuna sifa bainifu zinazoyatambulisha masimulizi yote (Propp, 1968; Olrik, 1992). Baadhi ya sifa za kina Propp na Olrik walizogundua ni pamoja na fomula ya kufungua masimulizi na fomula ya kufunga masimulizi, urudiaji miongoni mwa nyingine. Katika masimulizi ya utambaji hadithi ya kawaida, mtambaji anapoanza kutamba hadithi huanza kwa fomula ya kufungua hadithi na anapomaliza vivyo hivyo kuna fomula ya kumalizia. Hii ni sifa kuu ya fasihi simulizi. Ebrahim Hussein anaweka maonesho ndani ya utanzu wa fasihi simulizi ambao unaweka fomula ya mianzo ya hadithi na miishio ya vitendawili.

### 3.3 Fomula ya Ufunguzi Masimulizi na Dhima yake

Ebrahim Hussein kama mtunzi wa Kiafrika, ametunga tamthilia ya *Jogoo Kijijini* akitumia sifa muhimu za mianzo ya hadithi. Fomula ya kutanguliza hutumika katika masimulizi mengi ya Kiafrika. Dhima kuu ya mianzo hii ni kuwatayarisha wasikilizaji ili

waweze kujiandaa kwa masimulizi kuanza (Kipury, 1983). Fomula nyingi zimeonekana katika sehemu za mwanzo wa masimulizi na dhima kuu ya fomula hizi ni kujuza hadhira katika muktadha wa uwasilishaji wa masimulizi kile inatarajia kusikia (Manroe, 1972). Fomula hizi ni kama vile mtambaji anaposema, "hadithi hadithi!" huku mtambiwa akiitikia, "hadithi njoo".

Fomula ya kufungua hutekeleza majukumu kadha wa kadha yakiwamo: kushirikisha na kuleta mtambaji na wasikilizaji pamoja ili kuonesha kwamba wasikilizaji wako pamoja na mtambaji. Waaidha, fomula hii huteka na kuvuta makini ya wasikilizaji kwa lengo la kuwafanya kuwa tayari kumsikiliza mtambaji. Kadhalika, fomula huashiria mwanzo wa hadithi na kumtambulisha mtambaji hivi kwamba mtambaji anapoanza hadithi na hadhira kuitikia, inaonesha kwamba hadhira hiyo imekubali kutambiwa na hapo hadithi inaanza. Isitoshe, fomula huweka mpaka kati ya ulimwengu wa hadithi na ulimwengu halisi (Matei, 2011). Katika *Jogoo Kijijini* Hussein ametumia fomula ya kufungua kama ifuatavyo:

**Mtambaji hadithi:**
Paukwa
**Kiitikio:**
*Pakawa*
**Mtambaji hadithi:**
*Paukwa*
**Kiitikio:**
*Pakawa*
**Mtambaji hadithi:**
*Hapo kale, palikuwa na mkunazi*
**Kiitikio:**
*Naam twaiib…* (uk. 16)

Huu ndio mwanzo wa tamthilia ya *Jogoo Kijijini* sawia na mianzo ya ngano nyingi za Kiafrika katika masimulizi hasa ya Waswahili. Sawa na msikilizaji katika masimulizi ya ngano, msomaji au msikilizaji au yule anayeitazama tamthilia hii jukwaani, anaingiwa na hamu mara moja ya kutaka kujua habari za mkunazi huo mkubwa ambao umetajwa na mtambaji hadithi.

Ebrahim Hussein alizingatia baadhi ya dhima hizo alipokuwa anatunga tamthilia yake ya *Jogoo Kijijini*. Akizingatia dhima ya kuwashirikisha na kuwaleta pamoja wasikilizaji na mtambaji, mtunzi anauliza wasikilizaji 'paukwa' nao wasikilizaji wanajibu 'pakawa'. Katika kufanya hivi, mtambaji anadhihirisha bayana kwamba wasikilizaji wako pamoja naye. Kwa upande mwingine, iwapo mtambaji angeuliza 'paukwa' na hadhira ikose kuitika 'pakawa', mtambaji angekuwa na wasiwasi kwa sababu angefikiri kwamba hadhira haiko tayari kumsikiliza wala kushirikiana naye katika utambaji. Hii ingemzuia mtambaji kuendelea na utambaji wake.

Katika kutekeleza jukumu la kuvuta umakini au usikivu wa wasikilizaji, mtambaji huanza kwa kusema kwa hadhira 'paukwa!' ili kuizundua hadhira kuwa tayari kusikiliza. Nayo hadhira hujibu 'pakawa' kuonesha kwamba iko tayari kusikiliza. Ebrahim Hussein anaelewa kwamba ili kuteka fikra ya wasikilizaji wake anafaa awe na kitangulizi cha kuamsha mawazo yao. Mtindo huu unamtia hamu kuu msomaji, mtazamaji au msikilizaji. Mtu yeyote anayetambiwa namna hii anapata shauku ya kujua kitakachotendeka baadaye.

Dhima nyingine ya fomula ni kuweka mpaka kati ya ulimwengu wa hadithi na ulimwengu halisi. Katika kufanya hivi, mtambaji huikumbusha hadhira kwamba sasa imeingia katika ulimwengu wa ubunifu ili kuitoa katika ulimwengu halisi. Kwa mfano, mtambaji anaposema, 'hapo kale palikuwa na Mkunazi au Kitongoji' (uk. 12) hadhira inakubali au inaamini kwamba mambo yatakayotambwa ni ya kipindi cha kale na hayawahusu moja kwa moja japo huenda ikawa hadithi yenyewe ina wahusika wenye hulka kama zao. Kwa upande mwingine, iwapo mtambaji angeanza kwa kusema 'hapo jana kulikuwa na…', hadhira itahusisha kisa chenyewe na tukio halisi ambalo lilitendeka hiyo jana. Hali hii ingefanya hadhira kuona kuwa ni mambo halisi ambayo hutokea kila siku.

Fomula pia huashiria mwanzo wa hadithi. Kila utanzu au baadhi ya tanzu katika fasihi simulizi huwa na mianzo maalumu. Kwa mfano, kitendawili kina mwanzo wake mahususi ambao ni tofauti na mwanzo wa hadithi. Hadithi ina mianzo mbalimbali. Mianzo hiyo ni pamoja na 'paukwa pakawa', 'hadithi hadithi' na kadhalika (Wamitila, 2002). Ebrahim Hussein ametumia mwanzo wa 'paukwa' kwa lengo la kuonesha mwanzo wa hadithi yake. Mianzo hii hudhamiria kuonesha kwamba hadhira imekubali kutambiwa hadithi na hadithi huanza moja kwa moja.

Utamaduni wa simulizi haupotei au hauwezi kutoweka kwa kuingiliwa na fasihi andishi, badala yake usanisi hutokea ambapo masimulizi ya kimapokeo hudumu na kufyonzwa, kusilimishwa, kuenezwa na kuratibiwa upya ndani ya fasihi andishi (Obiechina, 1991). Kwa hiyo, Hussein ametumia mianzo hii kudhihirisha kwamba tamthilia hii imeandikwa kwa muundo wa fasihi simulizi ambao unaendelea kudumu licha ya kuingiliwa na fasihi andishi.

Katika fomula ya masimulizi ya Kiafrika, mianzo ya hadithi aghalabu huzua mgogoro, na mgogoro huu hupanda hadi kufikia kileleni katika sehemu ya kati na hatimaye kusuluhishwa katika sehemu ya mwisho (Kipury, 1983). Tamthilia ya *Jogoo Kijijini* imeanza kwa upeo wa chini ili kuvutia hadhira iweze kujumuika na kushirikiana na mtambaji katika masimulizi. Baada ya fomula ya kufungua, mtambaji anaanza masimulizi yake na *'hapo kale palikuwa na…*' (uk. 13) huku hadhira ikimsikiliza kwa makini. Nayo hadhira inaitikia, '*Naam twaiib'* (uk. 13) kama ishara ya kukubali kushiriki katika hadithi kama inavyodhihirika hapa chini:

**Mtambaji hadithi:**
Hapo kale, palikuwa na Mkunazi

**Kiitikio:**
*Naam twaiib*

**Mtambaji hadithi:**
Mkunazi mkubwa pita kiasi
Mkunazi huu ulikuwa unaitwa, Mkunazi-Rahmani…(kur. 13-14)

Baada ya hadhira kuitika *naam twaiib*, yaani kiitikio cha kuthibitisha kuwa kisemwacho kinakubalika au ni sawa, mtambaji huendelea na masimulizi yake katika upeo huo wa chini huku akielezea sifa za Mkunazi-Rahmani jinsi ulivyoweza kuzaa kunazi nyingi zisizo kifani na kila aliyeonja kunazi hizo alivyoingiwa na mahaba, huruma na ihsani.

Mtambaji anazidi kuhadithia jinsi homa kali au ‘mbuubuu’ mtamba-sumu ilivyokuja na kuuangamiza Mkunazi-Rahmani na baadaye ukavu ukazidi kwenye mji. Mtambaji anapotamba, hadhira inafuatilia hadithi, kisha mtambaji anatua. Huu ndio muundo uliotumika kutamba hadithi za Kiafrika. Mtambaji hutamba hadithi mfululizo kisha anatua kwa lengo la kuhakikisha iwapo yuko pamoja na hadhira au hadhira haisikilizi tena. Katika kufanya hivi, mtambaji hujenga taharuki ili kuvuta nadhari au umakini wa wasikilizaji wake na vilevile kuwashirikisha katika utambaji.

Baada ya mtambaji kuvuta makini ya hadhira na kuhakikisha kwamba iko pamoja naye, anaendelea na hadithi yake akiwa hapohapo kijijini. Katika kijiji kunawika Jogoo ambaye anaashiria mapambazuko. Kunapopambazuka unyayo unanyimwa uhuru wa kuliona jua. Wakati huohuo, unyayo unashtaki sikio ambalo limeshindwa kuyasikiliza mashtaka yake kuhusu kunyimwa kwake uhuru wa kuliona jua kila kunapopambazuka. Sikio lilikuwa la kufa halikuyatilia maanani mashtaka ya unyayo. Mtambaji anapofikia hatua hii, hadhira inaitikia kama ishara ya kumwambia fanani au mtambaji aendelee na hadithi kama inavyodhihirika hapa chini:

**Mtambaji hadithi:**
…Baina ya unyayo
Karibu na sikio
Aushi ya malalamiko
‘Nyayo litamka

‘Ewe sikio sikia;

Mimi mahabusu wa myaka
Wa k’yatu ulichonivika
Gizani ninadhoofika
Nataka ona juwa…

Nimechoka thama ‘mechoka
Najuwa Jogoo awika
Lakini mi nakwaruzika…

Lakini sikio,
Lilikuwa sikio la kufa…

**Kiitikio:**
Naam twaiib (kur. 15-17)

Hadithi inashika kasi wakati ambapo upeo wa chini unaimarika na kuanza kufunguka polepole ikielekea upeo wa juu yaani, sehemu ya kati. Mgani au mtambaji anaingiza hali ya taharuki na uchangamfu hadithini wakati ambapo anataka kujua hisia za hadhira yake. Katika hatua hii, mtambaji hutua na kuuliza hadhira kama ingetaka akomee hapo au aendelee na utambaji ili kumaizi iwapo hadhira bado iko makini. Dondoo lifuatalo linabainisha maelezo haya:

**Mtambaji hadithi:**

Kwani jogoo si Athumani
Anaijuwa yake thamani
Ya ile kazi yake aliyopewa
(*kituo)*
Je, niendelee?

**Kiitikio:**

*Endelea*

**Mtambaji hadithi:**

Niendelee?

**Kiitikio:**

*Endelea*

**Mtambaji hadithi:**

Au tukome hapo mpaka kesho?

**Kiitikio:**

*Wewe endelea*

**Mtambaji hadithi:**

Basi nitaendelea

**Kiitikio:**

*Naam twaiib.* (kur. 23-24)

Kulingana na dondoo hilo, katika fomula ya usimulizi mtambaji hujaribu kuishirikisha hadhira kwenye utambaji. Katika kufanya hivi, mtambaji huuliza maswali hapa na pale kwa njia ya kiitikio ili kujaribu kukaribia hali halisi ilivyo ya ushirikishwaji wa hadhira. Waaidha, mtambaji daima hujaribu kuiamsha hadhira au watazamaji kwa kurudia kuwauliza iwapo aendelee au akome na hadhira inatakiwa kujibu ‘Endelea! Mbinu ya uradidi ambayo mtambaji anatumia kwa hadhira inadhamiria kuondoa uchovu na kuwachangamsha wasikilizaji au hadhira (Kipury, 1983). Hii ni kwa sababu baada ya muda mrefu wa kutamba, hadhira inachoka na kukosa kuwa makini. Baadhi ya watambaji walitumia nyimbo na wengine mtuo wa kidrama na maswali. Kwa hiyo, Ebrahim Hussein aliamua kutumia muundo wa mtuo na maswali katika tamthilia yake kama inavyodhihirika hapa:

**Mtambaji hadithi:**

….Ingawa chache
Zilikuwa alama zake
‘Sabuni kuchomoza kwake
Mara ya pili kutokezea kwake
Ili nyayo jua kujitolea
Lakini
Hakuchoka asilani
Kwani jogoo si Athumani
Anaijuwa yake thamani
Ya ile kazi yake aliyopewa
*(kituo)*

Je, niendelee?
**Kiitikio**: Endelea… (uk. 23)

Muundo huu wa mtuo wa kidrama na maswali hutumika kumhakikishia mtambaji kwamba hadhira iko makini na hadithi ina mvuto kwao. Baada ya kuhakikisha, mtambaji anakuwa radhi kuendelea na utambaji wake.

Hadithi inakuzwa na kufikia upeo wa juu ambapo ajuza anaanza kumuelezea kijana asili ya kufika kwao pale kijijini. Kwamba yeye akiwa mtoto na watani wake walishika njia hadi wakafika kile kijiji. Walipofika pale walijenga nyumba juu ya kichuguu ambapo mlango uliliwa na mchwa waliokihamia kijiji hicho. Penye kichuguu palikuwa na mchwa ambao walikiangamiza kijiji. Kijana alipofahamu ukweli wa yale yaliyotendeka katika kijiji, aliamua kujitoa kafara kwa kujigeuza kuwa ng'ombe aendaye machinjoni huku akilia. Hadhira inaingiwa na taharuki kuhusu kitendo cha kijana huyu ambaye anatoa maisha yake (kur. 28-29). Tabia ya hadhira kushiriki kwenye usimulizi ni muundo pia wa kuhadithia ngano za Kiafrika. Hadhira huingilia kati na kushiriki ili kuhuisha masimulizi. Haya yanajitokeza kama ifuatavyo:

**Mtambaji hadithi:**
…Kijana kuushika ukweli
…Mabega yake wasaa mawili
Yalibeba madhambi ya ile njia…

**Kiitikio:**
*Masikini kijana masikini*
*Masikini lahaula masikini*
*Haya yote tanijilia lini?*
*Hata ye kujifanya ng'ombe alia…*

*Maisha yake hivi hivi*
*Kuyapoteza*
*Ndivyo hivi?*

*Au tabu 'lizopata*
*Mashaka yaliyomkuta*
*Dhiki zilizomkamata*
*Kuja hapa kuwa ng'ombe wa kafara*?...(uk. 28)

Baada ya hadithi kukuzwa na kufikia upeo wa juu, inaanza kushuka polepole kuelekea upeo wa chini. Kuna sheria mahususi ya kufungua na kufunga masimulizi. Sheria hii inashikilia kuwa masimulizi huanza kutoka upeo wa chini na kupanda polepole hadi upeo wa juu na kisha kushuka taratibu hadi upeo wa chini ambapo suluhu hutarajiwa kupatikana (Dundes, 1999).

### 3.4 Fomula ya Kuhitimisha Usimulizi na Dhima yake

Katika masimulizi hadithi haihitimishwi ghafla bali inaweza kutoa funzo, kuzawadi shujaa, kurejea kwa mtu fulani kwa heshima miongoni mwa mengine (Olrik, 1992). Katika utambaji wa hadithi, kuna fomula ya kumalizia utambaji wenyewe. Baadhi ya miisho huwapa wasikilizaji changamoto ili kuwafanya watafakari kwa kina ili

walifumbue fumbo lililomo katika hadithi (Chesaina, 1994). Hussein amemaliza hadithi zake kwa kitendawili ili kuwapa wasomaji na wasikilizaji wake changamoto ya kutafuta jibu la kitendawili. Kitendawili ni fumbo ambalo linaficha maana ya kitu ili kisijulikane kwa urahisi (Momanyi, 2001). Momanyi anaendelea kusema kwamba kitendawili cha masimulizi husimulia kisa na mwishoni mwa masimulizi hayo huhitaji fumbo kufumbuliwa. Ebrahim Hussein ameandika tamthilia ya *Jogoo Kijiini* kimafumbo ambapo mwisho wake inahitaji kufumbuliwa.

Ebrahim Hussein anapomaliza kusimulia hadithi katika *Jogoo Kijijini*, anatarajia hadhira kufumbua kitendawili katika hadithi. Hadhira inaposhindwa kung'amua fumbo katika hadithi, inaomba ufafanuzi. Kawaida hadhira inaposhindwa kutegua kitendawili, mtegaji hutaka apewe mji au zawadi yoyote ili aweze kutoa jibu la kitendawili chenyewe (Momanyi, 2001). Mtegaji ana uhuru wa kuukubali mji aliopewa au kuukataa ikiwa hajaridhika nao. Maelezo haya yanadhihirika kama ifuatavyo:

**Mtambaji hadithi:**
Basi hapa kadi tamati
Kadi tamati kalimati
Maneno yamenisaliti
Na kisa pia kimenikauka

**Kiitikio**:
Kisa tumekisikia
Utungo 'metueleza
Maneno 'metuingia
Ama maana hatujaambulia

**Mtambaji hadithi:**
Basi nipeni mji
**Kiitikio**
Nenda Kigoma
**Mtambaji hadithi:**
Hapana asilani
**Kiitikio**
Nenda Dodoma
**Mtambaji hadithi**
Hapana asilani
**Kiitikio:**
Nenda Dar es Salaam

**Mtambaji hadithi:**
Sasa maana tawatolea. (uk. 31)

Kutokana na maelezo ya dondoo hapo juu, mtambaji hadithi anapopewa miji mbalimbali ambayo hajaridhika nayo anaikataa hadi anapopewa mji ambao unamridhisha ndiyo anaukubali. Ebrahim Hussein ametumia muundo wa utegaji kitendawili anapoitamba

hadithi ambapo hadhira inashindwa kung'amua maana ya hadithi yenyewe. Hadhira inalazimika kutaka kufumbuliwa maana ya fumbo katika hadithi. Lengo kuu la muundo huu wa kuhitimisha ni kuifanya hadhira iwe na uchunguzi mahiri wa mazingira yao mbali na kuifunza aina mbalimbali za mahusiano katika jamii inamoishi. Pia, ni njia ya kuipumzisha au kuituliza hadhira ambayo ilikuwa imetulizana na kuwa makini wakati wote wa masimulizi.

Fomula ya kuhitimisha inatekeleza dhima nyingi katika masimulizi (Matei, 2011). Dhima hizi mahususi ni kama zifuatavyo: fomula ya kufunga huonesha mwisho wa hadithi na kuwa kitulizo kwa wasikilizaji ambao wamechoka. Aidha, fomula hii hutoa funzo au adili kwa wasikilizaji au wasomaji. Kadhalika, fomula ya kufunga huwa kama changamoto kwa wasikilizaji. Pia, fomula hii huitoa hadhira kutoka ulimwengu bunifu hadi ulimwengu halisi, na mwisho fomula humpisha fanani na shughuli inayofuata kwa kuwa kazi ya utambaji imekamilika.

Ebrahim Hussein katika utunzi wake wa tamthilia ya *Jogoo Kijijini*, ametumia fomula ya kufunga ili kuonesha mwisho wa hadithi. Mtambaji katika tamthilia hii anaposema ' *…basi hapo kadi tamati, kadi tamati kalimati'* (uk. 31) wasikilizaji au hadhira hufahamu kuwa hadithi imefikia kikomo. Kwa vile hadithi yenyewe ni kitendawili na ni changamano zaidi, hadhira inaomba mtambaji aifafanulie maana ya hadithi hiyo ili iweze kuielewa bayana.

Fomula ya kufunga huwa kitulizo kwa wasikilizaji ambao walikuwa wamechoka kwa kuwaondolea taharuki na kuwapa maana kuhusu kisa kilichokuwa kinasimuliwa (Matei, 2011). Ebrahim Hussein ametumia kimalizio katika hadithi yake ya *Jogoo Kijijini*. Baada ya mtambaji kufika tamati katika tamthilia ya *Jogoo Kijijini*, hadhira inaomba mtambaji aieleze maana ya kitendawili ili ipate nafuu. Wasikilizaji katika *Jogoo Kijijini* wanamwambia mtambaji kwamba, '*kisa tumesikia, utungo 'metuelea, maneno 'metuingia, ama maana hatujaambulia'* (uk. 31). Kwa hiyo, hadhira ina hamu ya kupata kitulizo baada ya kusikiliza hadithi.

Fomula pia hutoa funzo au adili kwa wasikilizaji. Hadithi huweza kutoa funzo kwa kutumia methali, kitendawili au msemo ambao hutoa muhtasari wa maadili katika hadithi (Matei, 2011; Lyimo, 2017). Katika tamthilia ya *Jogoo Kijijini*, mtambaji anamaliza hadithi kwa kitendawili japo hajaweza kutoa maana ya kitendawili. Huu ni muundo wa kipekee wa Ebrahim Hussein ambao ameutumia katika utunzi wa tamthilia ya *Jogoo Kijijini*. Muundo huu unampa msomaji changamoto ya kutafakari kwa kina zaidi. Kwa vile mtambaji hajatoa maana ya kitendawili, hadhira inamsihi aieleze maana yake.

Kadhalika, fomula ya kufunga pia huzua changamoto kwa hadhira. Kuna hadithi ambazo ni changamani zinazohitaji ufafanuzi wa kina ili maana iweze kujitokeza. Hadithi katika *Jogoo Kijijini* ni changamani zaidi. Hata mtambaji anapofika mwisho wa hadithi yake, wasikilizaji wanashindwa kung'amua maana ya hadithi yenyewe. Hali hii ndiyo inayowafanya wasikilizaji kumsihi mtambaji awape maana ya hadithi yenyewe. Wasikilizaji wanahisi kwamba hadithi ni changamano kuielewa. Hali hii huipa hadhira uhuru wa kutathmini au kutoa hukumu badala ya kumwachia mwandishi peke yake (Lyimo, 2017)

Fomula ya kufunga pia huitoa hadhira kutoka ulimwengu bunifu hadi ulimwengu halisi (Matei, 2011). Wakati wote mtambaji anapokuwa akitamba, hadhira inakuwa katika ulimwengu bunifu kwa sababu mtambaji alianza na '*hapo kale palikuwa na*…' (uk. 13). Hadhira inaposikia maneno hayo, inaingia katika ulimwengu wa ubunifu. Wakati mtambaji anapomaliza kutamba, hadhira inarudi tena katika ulimwengu halisi wakati

inaposikia maneno '…*basi hapo kadi tamati'* (uk. 31). Maneno haya yanaashiria mwisho wa hadithi.

Aidha, fomula ya kufunga hupisha shughuli inayofuata. Baada ya utambaji kukamilika, ni wazi kwamba shughuli nyingine ingefuata. Lakini hili halingetokea bila ya kidokezi au fomula ya kupisha shughuli hiyo. Mtambaji anapoieleza hadhira kwamba, '*Basi hapa kadi tamati. Kadi tamati kalimati. Maneno yamenisaliti. Na kisa pia kimenikaukia*'. (uk. 31), bila shaka hadhira inabaini kwamba utambaji umekamilika na kwa hiyo inaweza kufanya shughuli nyingine. Kwa hiyo, fomula ya kufunga hutumika kupisha shughuli nyingine kufanyika au kumpisha mtambaji anayefuata.

### 4.1 Hitimisho

Makala hii imehakiki fomula ya kisimulizi katika tamthilia ya *Jogoo Kijijini*. Mihimili ya Nadharia ya Fomula ya Kisimulizi ya Propp (1968) na Olrik (1992) imetumiwa kuonesha fomula hizi. Katika uchanganuzi huu, imebainika kwamba Ebrahim Hussein ametumia fomula ya kisimulizi katika tamthilia yake. Tamthilia ya *Jogoo Kijijini* inawasilishwa katika muundo wa fasihi simulizi. Tamthilia hii imechota malighafi yake kutoka sanaa ya Kiafrika iliyohusisha kuchunguza na kusaka, kuendeleza na kufanya upya utendaji halisi wa utamaduni wa Kiafrika ambao ulikuwa ukiendelea katika Afrika Mashariki hasa katika nchi ya Tanzania. Kutokana na uchanganuzi huu, imebainika kwamba tangu mwisho wa miaka ya sitini katika karne ya ishirini, Hussein anaonekana akiacha mwelekeo wa Brecht ambao alitumia katika tamthilia yake ya awali ya *Mashetani* na kutumia umbo la masimulizi ya Kiafrika kama ukweli dhahiri wa Uafrika. Majaribio haya yameleta upya katika fani ya tamthilia ambayo ilitegemea zaidi usanii wa vitendo na usemaji tu.

## Marejeleo


Chesaina, C. (1994). *Literature of the Kalenjin*. Nairobi: East Africa Educational Publishers.

Chiraghdin, S. (1976). katika Utangulizi wa *Jogoo Kijijini* na *Ngao ya Jadi*. Nairobi: OUP.

Dundes, A. (1999a). *Varia Folklorica*. Paris: Moulton Publishers.

Dundes, A. (1999b). *International Folkloristics*. Oxford: Rowman and Litlefield Publishers.

Hussein, E. (1976). *Jogoo Kijijini na Ngao ya Jadi.* Nairobi: Oxford University Press.

Kipury, N. (1983). *Oral Literature of the Maasai*. Nairobi: Heinemann Educational Books (EA) Ltd.

Lord, A. (1960). *The Singer of Tales*. Cambridge: Havard University press.

Lord, A. (2000). *The Singer of Tales*. Cambridge: Havard University press.

Lyimo, B. (2017). "Dhima ya Mianzo na Miisho katika Nathari za Kiswahili za Fasihi ya Watoto: Mifano kutoka Riwaya na Hadithi za Kiswahili za Watoto Nchini Tanzania," katika *Kioo cha Lugha*,15: 89-107.

Miruka, O. (1999*). Oral Literature*. Nairobi: Acacia Publishers Ltd.

Mlama, P. (2005a). "Hali ya Sanaa za Maonyesho Tanzania," katika: *Makala za Semina yaKimataifa ya Waandishi wa Kiswahili.* Dar es Salaam: TUKI. Kur. 186-196.

Mlama, P. (2005b).“Utunzi wa Tamthiliya katika Mazingira ya Tanzania,” katika: *Makala za Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili.* Dar es Salaam: TUKI. Kur. 206-225.

Mulokozi, M.M. 2017). *Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili: Kozi za Fasihi Vyuoni na Vyuo Vikuu*. Dar es Salaam: KAUTTU.

Nandwa, J. and Bukenya, A. (1983). *African Oral Literature for Schools*. Nairobi Longman Publishers.

Njogu, K. na Chimerah, R. (2011). *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu*. Nairobi: JKF

Obiechina, E. (1991). *Language and Themes: Essays on African Literature*. New York:Howard University Press.

Propp, V. (1968). *Morphology of Folktale*. Texas: Universiy of Texas Press

Propp, V. (1984). “Introduction”. *The Theory of Folklore*. University of Minnesota: University of Minnesota Press. Pp ix.

Propp, V. (2008). *The Literary Encyclopaedia: Exploring Literature, History and Culture.* Los Angels: University of California Press.

Wamitila, K. (2002). *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele Vyake*. Nairobi: Phoenix Publishers.

Wamitila, W. (2010). *Kanzi ya Fasihi: Misingi na Uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi: Vide-Muwa Publishers Ltd.

Wamitila, K. (2012). *Kichocheo cha Fasihi Simulizi na Andishi*. Nairobi: Focus Books.